



## REPUBLIC OF KENYA

### COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

#### THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

##### THE HANSARD

**Tuesday, 19<sup>th</sup> November 2024**

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

*[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]*

##### PRAYER

##### STATEMENTS

##### STATUS OF KITSAMINI MKWAJUNI AND MWAKUWAWA PRIMARY SCHOOL ECDE PROJECTS IN MARIAKANI WARD

**Hon. Rashid:** Mr. Speaker, I rise in Response to a Statement sought by hon. Koki from the CECM (County Executive Committee Member) Education and ICT Department regarding Kitsamini Mkwajuni and Mwakuwawa Primary School ECDE project in Mariakani Ward. The Response is as follows: -

- The aforementioned projects were Ward Development Projects for the financial year 2020/2021.
- Both projects were awarded to Nyange Mjomba Enterprises.
- Both projects were done up to the gable stage (awaiting roofing).
- The contractor submitted a payment certificate while at the substructure level, which was paid. However, the subsequent certificates for the amount of works done up to the gable

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

stage, one for Mwakuwawa and another for Kitsamini Mkwajuni respectively have not yet been paid.

- Due to the delayed payments, the contractor halted construction works and has stated that they will only resume work upon receiving payment.
- Consequently, both projects remain stalled.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Hon. (Ms.) Koki, the Response has been made, and we want to hear whether you are satisfied or not.

**Hon. (Ms.) Koki:** Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity to respond to the Response given by hon. CECM Education. I stand here on behalf of the people of Mariakani and without any fear and doubt to say that I am not satisfied with this Response because, one; you cannot give a Response of two stalled projects in a bullet form in five lines.

Two; as a department, when you tell the people that due to delay of payment that is the reason why these projects have stalled, I was expecting an explanation. What the Department is doing so that we do not have any stalled projects? This is not only for Mariakani but for any other Wards in Kilifi County. We cannot talk about stalled projects because of payments. What is the Department doing to make sure that they liaise with the Department of Finance and Treasury to make sure that we do not have any stalled projects?

I followed up on these two projects myself from the Department of Education and Finance and two certificates were raised for payments, but they have not been paid until today. Is it me or the Department to make sure that they follow up so that these contractors can go back to the ground and do their work? I will tell you, Mr. Speaker, Sir, these projects were four; it was Kitsamini and Mwakuwawa, Vuma and Kadzandani Primary Schools. Vuma and Kadzandani projects were cancelled and were awarded again, and these two ECDEs were ready for use.

Just the other day, I took furniture for those ECDEs, and these were projects for the same year. Now the people of Kitsamini and Mwakuwawa are complaining because their ECDEs are not ready and here the CECM is telling us that the projects have stalled because of non-payment. It is not the problem of the people of Mariakani; we need the ECDEs to be done. I am not happy with this Response. Can we get the correct Response so that when I go back to Kitsamini and Mwakuwawa, I will give them the correct information that their ECDEs are going to be cleared and come next year, they will have somewhere to go to School?

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Hon. Koki is not satisfied with the answer. So, I want to commit this matter back to the Committee to make investigations into the same and bring a satisfactory answer to this honourable House.

**Hon. Zia:** Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipa hii fursa. Kidogo naendelea vizuri, Bw. Spika, japo nimekosekana kwa muda kwa sababu ya hali yangu ya kiafya lakini saa hii nimeanza kupata afueni japo sijakuwa sawa.

Kulingana na haya majibu ambayo yamesomwa na Mwenyekiti na pia jinsi aliyeuliza hili swali hakuridhika kwa sababu kuna baadhi ya miradi ambayo tuko nayo katika sehemu zetu, basi ni kusema kwamba naungana moja kwa moja na mheshimiwa ambaye ametoka kwa Sakafu, mheshimiwa Koki ya kwamba kweli, mheshimiwa Spika, kuna shida mahali kwa sababu ndio niliongea mwanzoni mwa mwezi wa saba ya kwamba hii miradi iliyokwama iko kila mahali. Hata mimi niko nayo hiyo miradi ambayo imekwama na ukiuliza swali unajibiwa namna ambayo hairidhishi.

Nilizungumza wakati ule wa mwezi wa saba nikasema kwamba kuna baadhi ya miradi ambayo iliorodheshwa kwamba imepewa kima cha pesa fulani, japo imekwama, lakini katika

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

bajeti ikatolewa wakati wa *Supplementary*. Kuna wakati niliuliza lile swali. Ni pesa ngapi ambazo zimeweza kutumika za mwaka wa 2023/2024? Nafikiri jibu lililotoka hapa ni kwamba katika ile miradi ambayo pesa zake ziliweza kutolewa, unaiona kwamba imetokea tena. Imeonyeshwa tena katika yale majibu ambayo alikuwa ameleta hapa. Mheshimiwa Spika, pale kama hatutakuwa makini sisi waheshimiwa na kuungana kwa pamoja, watu wetu wataendelea kuumia.

Hii miradi ambayo imekwama haiendelei lakini utaipata kwamba imetengewa pesa. Halafu baadaye utaona kwamba pengine kama ni *Supplementary*, hizo pesa zinatolewa na ukiuliza swali utapata kwamba ati *contractor* hajapatikana; mara huyo mwanakandarasi amepewa lakini bado anashughulikia hiyo kitu. Mwaka umeisha na baadaye unapata kwamba imepelekwa kwa ule muhula mwengine wa pesa ambao unakuja.

Naogea nini? Nasema ya kwamba, *Executive* ni ibadilike na ifanyie kazi wananchi wa Kilifi la sivyo, sisi hatutaonekana kwamba tunafanya ile kazi ambayo inapaswa. Kule nyanjani ile miradi bado iko hivo katika ile serikali ambayo iliweza kutoka mpaka saa hii bado miradi inaendelea. Kwa mfano tu, juzi mliona kwa mitandao, saa hii hata hizo habari zilitapakaa Kenya nzima kuhusu ile Shakahola *Dispensary*. Shakahola *Dispensary* iko kwa *financial year* ya ...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Samson (Zia), tuchangie kulingana na mada. Toa mfano lakini tuende kwa mada ambayo tuko nayo. Tusiende na mifano ambayo iko nje.

**Hon. Zia:** Ndio nakutolea hiyo mifano na hizo pesa zilionyeshwa, hata *financial year* ilionyeshwa, na hata kuna shilingi *five million*, zinaonyesha. Lakini, hiyo *dispensary* haitengenezwi mpaka saa hii. Kuna Adu *Dispensary* mpaka saa hii bado haijafanya kazi. Kuna barabara hii ya kutoka Kibao cha Fundisa hadi Adu bado haijatekelezwa. Ni baadhi ya miradi ambayo iko hapo na zile wadi nyengine nyengine ambazo ziko. Haifanywi haiendelei. Ukiuliza maswali, majibu... Mheshimiwa ameuliza swali zuri sana lakini yale majibu ambayo yameorodheshwa hapo hayaridhishi. Hayaridhishi, mheshimiwa Spika, na hii ndiyo ambayo inatuchapa sisi. Kwa hivyo, ni lazima wabadilike na kama hawatabadilika, kuna shida. Ni lazima tusimame kidete na tuweze kusukuma *Executive* iweze kutekeleza hii miradi la sivyo, tutakuja kujuta hata sisi pia wakati huo ukifika. Asanteni sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Asante. Kwanza, tukupe pole mheshimiwa kwa yale ambayo uliyapitia. Umekuwa katika maombi yetu na hata saa hii bado tunaendelea kukuombea. Asante. Kuna mheshimiwa mwengine ambaye angependa kuongea? Pengine unyoshe mkono ili tuweze kukusaidia. *Yes, Chairman.*

**Hon. Rashid:** Thank you, Mr. Speaker. Indeed, it is so unfortunate that Members are giving such reactions and they are not satisfied with the Response. Again, it is so unfortunate, Mr. Speaker, that if the Deputy Majority Leader cannot be satisfied, what about the others? Mr. Speaker, it is true. I agree with the Deputy Majority Leader. There have been overwhelming complaints that people are not satisfied with the Responses. I was very keen while I was reading the Response and I noticed that the Deputy Majority Leader was in a deep reverie, but the Englishman said, if you live by the sword, you die by the sword. Mr. Speaker, allow me to read the second Response.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): There is a point of intervention. I think the matter has not been exhausted yet. Some Members still want to make contributions. Yes, you are free.

**Hon. (Ms.) Koki:** Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi. Mwenyekiti ambaye yuko kwa Sakafu kwa uhakika sijui alikuwa anapatiana *Response* ama alikua anasemaje. Hii

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

shida ambayo tuko nayo sio ya Serikali ya Kaunti ya Kilifi bali ni ya kila mtu aliye Kilifi ikiwa hata yeye ni mmoja wao kwa uhakika ile *Statement* ambayo ameizungumza saa hizi ni ya kukejeli na yeye yuko katika serikali maana alichaguliwa na walio wengi ambao ndio wengi katika hili Bunge. Akisema mimi niko kwa serikali, je wale wengine?

Yeye yuko katika ile serikali mimi niliyoko. Kwa hivyo tusilete siasa na tusilete kejeli kwa mambo ambayo yanagusa mwananchi hususan mtoto wa Kilifi. Kama yeye pia hajatosheka na yale majibu ambayo Waziri ameyazungumza, kama Mwenyekiti, aseme pia yeye hajatosheka; wataenda kurekebisha na tupate majibu yanayostahili. Tuwache kejeli na tuwache kuzungumza mambo mengi. Nikiwa ndani ya serikali, yuko katika ile serikali ambayo mimi niko. Asante.

*(An hon. Member spoke off record)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mwenyekiti, hebu kaa kwanza. Nataka ukae tafadhali. Nafikiri umeelewa kile ambacho mheshimiwa amekizungumzia na ni vizuri tujue ya kwamba swali lililoulizwa lilikuwa ni kwa niaba ya wana Kilifi wote. Mariakani iko Kilifi na sisi sote tunafanya kazi na Bunge hili linafanyia kazi wananchi wa Kilifi. Kwa hivyo, tujue kwamba tukisema kwamba mdogo wa waliowengi hajatosheka na jibu kwa sababu yeye yuko upande wa serikali sio sawa sawa. Nataka *Chairperson*, tuliwachie hilo jambo hapa.

*(Loud consultations)*

Waheshimiwa, naomba kama mheshimiwa Spika anaongea, musikilize; hatujibizani. Kwa hivyo, kama kuna mheshimiwa yeyote ambaye angetaka kuifanya *contribution* kabla tu *commit* hii *matter* kwa *Committee*. Mheshimiwa Baya (Stephen).

**Hon. Stephen:** Asante sana, Spika, kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa mchango wangu pia kwa niaba ya wale watu ambao nawawakilisha pale Bungeni. Pia mimi namuunga mkono mheshimiwa Koki ya kwamba hajatosheka na majibu ambayo amepewa hapa Bungeni kuhusiana na miradi ambayo imekwama. Kwa hakika, mheshimiwa Spika, miradi imekwama Kilifi Kaunti nzima hususan upande wa madarasa. Kuhusiana na madarasa, mimi pia pale Gongoni nimeathirika vibaya sana. Niko na madarasa mawili mahali kunakoitwa Katsemerini. Hayo madarasa yamekuwa muda mrefu hayajaisha. Niko na madarasa mawili Sabasaba ndani ya Gongoni. Hayo madarasa yamekwama hayajaisha. Niko na madarasa mawili Povuni; hayajaisha. Niko na madarasa mawili mahali kunaitwa Kadzaheni ndani ya Gongoni ambayo hayajaisha.

Mheshimiwa Spika, kila wakati ukienda kwa wizara husika kuuliza maswali kuhusu haya madarasa yatamalizwa lini, yale majibu unapewa pale ni majibu ambayo hayaeleweki. Kule nyanjani wale wananchi ambao walituchagua na kutuweka kwa serikali hii waliamini kuwa mheshimiwa Gavana atakapolingia atafanya mabadiliko akishirikiana na sisi hapa Bungeni. Kule nyanjani wale wananchi yale mabadiliko hawayaoni kwa sababu mradi unakaa zaidi ya miaka miwili bila kuisha. Watoto wanasoma chini ya mti; watoto wanasoma chini ya kanisa kwa sababu wameomba na sisi tukaona tuwawekee madarasa ili waweze kusoma mahali pazuri lakini unakuta miradi ile imekwama.

Ningependa kueleza Wizara ya Elimu ambayo iko hapa iweze kujizatiti kidogo kwa sababu upande huo unalemaa. Hii Miradi ilipowekwa pale kulikuwa kuna pesa zimetengwa za kuwa hii miradi ikiisha pesa ziko pale lakini kile kitu nashangaa hatujui ni kitu gani. Hizi pesa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

baada ya kuwekwa kwa yale madarasa ni kitu gani ambacho kimekuwa mbeleni hali ya kuwa haya madarasa hayawezi isha? Tunajua mwanakandarasi akishindwa, ni jukumu la Wizara ya Elimu kutafuta mwanakandarasi mwingine ili aweze kutengeneza haya madarasa.

Wananchi kule nyanjani ambao hawaelewi wanatupiga vita sisi wajumbe wao kuwa pesa zimetolewa kujenga madarasa Katsemerini lakini mheshimiwa wetu inaonekana amechukua pesa hizi na amekula. Hawajua zile *process* ambazo zinaendelea; ni lawama kule chini. Hawajui kuna *process* gani hata mimi pesa sigusi ni mwanakandarasi ajenge na aende akalipwe kule; wao hawajui. Mheshimiwa Spika, wananchi wanajua kuwa mheshimiwa wao amepewa pesa na amekula na hata uwaeleze namna gani hawawezi kuelewa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba hii Wizara iweze kujizatiti kidogo. Kuna lawama nyingi sana na haya malalamishi naongea hapa niko na uhakika hata kwa Wadi nyingine malalamishi haya yako. Sisi waheshimiwa ambao tumechaguliwa hapa na tunawakilisha wale wananchi, tusikubali wizara fulani ifanye tuonekane hatufanyi kazi na serikali mzima na Gavana wetu pia aonekane hafanyi kazi kwa sababu ya watu fulani ambao wanazembea kazini.

Ningeomba kila Wizara ifanye kazi kwa bidii na ihakikishe inafanya kazi kulingana na wananchi chenye wanapenda. Tukifanya hivyo basi wananchi baada ya miaka mitano wakiona yale mabadiliko ambayo yamefanyika ndani ya Kilifi watakuwa na imani na hii Serikali na watakuwa na imani na sisi viongozi ambao walituchagua. Hivi sasa imani zimeisha; miaka miwili imeisha na madarasa yako pale. Hivi nikiweka mkutano Katsemerini ama Sabasaba ni kutukanwa tu na wananchi na serikali yetu ya Kaunti ni kutukanwa tu kwa sababu ya watu ambao wanazembea kwa kazi yao.

Mheshimiwa Spika, ningependa hii Wizara iweze kuangalia vizuri. Ninamuunga mkono Mheshimiwa Koki kwa yale amesema. Haya majibu ambayo wametupa hapa hayawezi kuridhisha; ni watupatie majibu ya *projects* zote ambazo zimesimama ndani ya Kilifi Kaunti hususan Wizara ya Elimu. Watuambie hii miradi inaisha lini na imepangiwa nini. Saa hii tunamaliza mwaka na tukirudi ni mwaka wa tatu na miradi haijaisha. Huenda tukaenda mpaka miaka mitano ikaisha. Je, tutaambia nini wananchi? Mimi nataka kuishia hapo lakini Wizara iweze kujipanga vizuri na iweze kufanyia kazi wananchi wa Kilifi ili kwamba tusipakwe matope sisi.

Mheshimiwa Spika, kila ukiingia kwa ofisi ukiwauliza wanakupa majibu ni kama kesho kutafanyika kitu, lakini ikifika kesho hakuna chenye kimefanyika. Mimi naishia hapo lakini hili jambo linapiga vita serikali yetu ya Kaunti na sisi waheshimwa ambao tuko hapa hatutakubali. Ikifika mahali kila mmoja alaumiwe na sehemu yake. Nasema kwa hayo machache, Mwenyezi Mungu atubariki sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Asante sana, mheshimiwa Baya Mwaro (Stephen). Endelea, mheshimiwa Twaher.

**Hon. Twaher:** Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Mimi ninashukuru kwamba leo tumejumuika hapa ili kutekeleza majukumu yetu. Hii *Statement* ya kuwa kuna *stalled projects* ambazo kwamba zenye zimeidhinishwa hapa ni za Mariakani, nataka kukubaliana na mheshimiwa wa Gongoni kuwa *stalled projects* ni nyingi hata kwangu kuna *stalled projects* ya ECDE inaitwa Kajajini; mpaka sasa haijakamilika. Imemaliza miaka saba haijakuwa *handed over* kwa *community* imebidi wanafunzi wanasoma kwa hiyo *stalled project* hivyo hivyo na haijakamilika.

Hili swala la kuelezewa kuwa mkandarasi hajamaliziwa sijui pesa zake is *the same story*. Pale yule mkandarasi amebakisha shilingi milioni moja lakini milango hajaweka, rangi hajapaka

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

na hata *ramp* hajatengeneza. Mheshimiwa Spika, imelazimu wananchi waingie kuanzisha masomo vile vile hali ilivyo. Ni jambo la kusikitisha kwamba Mwenyekiti ambaye tuko naye hapa ambaye anatakikana ajukumike yeye ni mwalimu *by profession* na inafaa awe mzazi wa kwanza wa huzuni wa maswala kama haya. Nataka ku *point* mfano wa muhimu sana, huyu mheshimiwa Koki yuakaa kwa Kamati ya Bajeti...

*(An hon. Member spoke off record)*

Mheshimiwa Spika, nataka anipe nafasi nielezee alafu a *interject*...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Point of information from hon. Mapenzi. Just a moment...

**Hon. (Ms.) Mapenzi:** As a parent, I think the Response is not from the Chairperson; it is from the Department. Thank you.

**Hon. Twaher:** *Thank you, so much hon. Mapenzi. That is very clear. Thank you very much, for that clarity. As I was saying it was very important to wait for me to finish my statement.*

Nataka kuendelea kwa Kiswahili, mheshimiwa Spika. Kuna kitu muhimu nilikuwa nataka kuelekeza. Mheshimiwa Spika, kuna shule inaitwa Cleopatra ambayo iko Malindi *Town Ward* na iko hapa *Municipal Stadium*, ni *Municipal Stadium ECDE*. Hii shule ilikua *dilapidated*, yaani nikunukuu kwa neno la Kiingereza yaani imevunjikavunjika mpaka wale wanafunzi wakawa hawawezi kusoma katika hiyo shule. Hili tukio limetokea sasa ni mwaka mmoja na nusu; wanafunzi wa ile shule wamehamishwa wameletwa shule inaitwa Sir Ali ECDE ambayo iko katika Wadi yangu na imeleta msongamano katika ile shule. Jambo la kusikitisha ni Mwenyekiti wa Kamati hii ni mheshimiwa wa Wadi hiyo. Ndio swala kwa sababu sisi tuko hapa kuwakilisha wananchi katika maswala yote ya nyanja zote na hapa twazungumzia nyanja ya elimu, mheshimiwa Spika.

Hili swala mimi lilinikera kwa sababu watu wa hii Idara walipoleta mswada wao hapa wa bajeti hawakuiwekea pesa hiyo shule; haikuwa na fedha ya aina yoyote ya kurekebisha lile tatizo. Katika maswala ya kupanga bajeti, mimi nilielekeza hiyo hoja ambayo ile haikuwa Wadi yangu nikasema kuna shule imevunjika na iko hali mbaya; wanafunzi mpaka wamehamishwa. Katika Kamati ya Bajeti ambayo mheshimiwa Koki pia yumo, akasema hiyo ni hali ngumu sana kwa sababu wale ni watoto wadogo. Naelezea zile hali kwa sababu hii *Response* ambayo imeletwa kutoka kwa Wizara ...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Twaher, naomba ukae. Vile unavyoendelea kuzungumza tunatoka nje ya mada na naelewa ya kwamba uko na *point* ya *ku-prove* lakini tunaomba uzingatie kwamba tunazungumzia swala la jibu lililotoka kwa swali lililotoka. Tubaki pale pale.

**Hon. Twaher:** Asante kwa muelekeo.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Halafu uangalie muda wako.

**Hon. Twaher:** Asante sana. Nilikuwa naelekeza hii Hoja kwamba haya majibu ambayo yamekuja ni majibu ya kusikitisha sana na wale watoto ambao sisi tunawashughulikia ni watoto wadogo na hizi shule zikikaa katika hali ile sisi sote hapa haturidhiki na tukifika hapa ni lazima tushirikiane katika maswala ya kuhakikisha huduma nzuri zimefanyika. Nilikuwa naelezea ile hali halisi. Hivi sasa tunavyozungumzia tuliweka zaidi ya shilingi milioni nne katika hiyo shule na sasa hivi madarasa yatawekwa ili ile shule irekebishwe na masomo yazidi kuendelea.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sisi tunalizungumzia swala hili kwa uchungu kwa sababu katika bajeti kunawekwa *programmes* za kujenga shule nyengine na kuna nyengine ambazo zime-*stall*. Hawa watu katika hii Idara wanatuletea miradi mipya na wakati kuna miradi imekwama kwa sababu wanaona pengine hii miradi ikiwekwa lazima waeke miradi mingine na hii mingine bado haijamalizika. Hii *Response* tumeletewa haitukinaishi sisi kuonyesha kwamba utendakazi utafanyika, sisi tulitarajia watuambie ni hatua gani na itachukua muda gani hii *project* imalizike. Kinachonisikitisha mimi ni kwamba sisi sote hapa ni wajumbe na leo ni *area* yako, kesho ni *area* yangu. Kwa upande wa mambo ya miradi lazima tusimame pamoja kama Bunge. Usiwe wewe katika Kamati kwa sababu ni Mwenyekiti unataka kujipendekeza kule ujionyeshe kwamba wewe uko pamoja na Idara. Hili jibu halituriidhishi!

*(Loud consultations)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa, muda wako umiesha.

**Hon. Twaher:** Asante.

*(Loud consultations)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Order! Mheshimiwa Tete.

**Hon. Tete:** Asante, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Naunga mkono mheshimiwa Koki kwa kusema kwamba hajatoshelazwa na majibu ambayo yemeletwa na Waziri wa Elimu. Mimi nikisimama hapa sina mradi wowote wa Kitengo cha Elimu ambao uko pale kwangu ambao umesimama na napenda kushukuru kwa hilo kwa sababu si kwamba ni mzuri au ni bora kuliko wenzangu. Chenye kinaendelea iwapo kuna Wadi ambayo ina shida kama ya mheshimiwa Koki na hakuweza kubahatika kuleta *Statement* kwa Waziri aeleze ni kwa nini mambo kama haya yanaendelea lakini mheshimiwa mwengine amefaulu, jambo hili linastahili kuzungumziwa kwa mapana.

Cha kwanza, tunawakilisha wadi na tuko hapa kufanyia kazi wananchi wa Kilifi. Kwa hivyo, tunaposimama na Hoja ambayo imeletwa na mwakilishi Wadi ambaye ni mwakilishi wa wananchi, kile kitu ambacho ningomba tuangazie ni kwamba tunapewa mstari wa mbele kuona kwamba tunasikitikia wananchi kujua ni njia gani tutawapeleka mahali pa sawa.

Mimi nikiwa mwakilishi Wadi wa Shimo la Tewa, ninapenda kusimama nikisema tumefahamishwa mengi kupitia kwa waheshimiwa ambao wamesimama wakizungumzia ya kwamba twende moja kwa moja kwa majibu yaliyopeanwa katika *Statement* iliyoapeanwa na Waziri lakini naona kuna kitu ambacho kimeenda kombo na, mheshimiwa Spika, hukuweza kutukinga. Mheshimiwa anaposimama kusema ya kwamba ukiua kwa upanga, utauawa kwa upanga hii ni kama ni *tit for tat* ya sisi kwa sisi na ninaona kama ambaye si lugha ambayo tunastahili kutumika kujadili Hoja. Ninaomba ikiwa kuna mwenzetu ambaye anaumia mahali na amesimama kusema kwamba hili jambo haliendi vizuri tulitafakari kwa kina na tusimame tukijua ya kwamba kuna uhitaji unatakikana kupatikana jawabu.

Naunga mkono kutoridhika kwa mheshimiwa Koki na haya majibu na nataka kusema kwamba kabla ya kusimama kuomba nafasi ya kuzungumzia Hoja, angalia kile ambacho kimewekwa mezani kinafafanua nini kuhusu kwako na kwa mwenzako. Kwa haya mengi na machache, mheshimiwa Spika, nasema asante.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. (Ms.) Mariam:** Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipa fursa hii. Nami pia niungane na wenzangu kwa kusema kwamba yale majibu yaliyoletwa kutoka kwa Waziri ni majibu ambayo hayaridhishi. Hii ni kwa sababu hayajapeana jibu. Kusema kuwa mkandarasi aliwacha kazi, hilo si jibu kwa sababu kuna sheria ambayo inampatia muda mkandarasi katika utekelezaji wa kazi yoyote ile. Baada ya huo muda ikiwa mwanakandarasi yule hajaimaliza vile vile kama Wizara ama Serikali ina ruhusa ya kuhakikisha kuwa huyu mkandarasi amepokonywa hiyo kazi na akapewa mkandarasi mwingine ili iendelee.

Pia tukiangalia katika maswala ya miradi ambayo imekwama, hii ni miradi ambayo huwa katika bajeti imewekewa pesa. Tunavyojua swala zima la mduara wa bajeti ni kuwa tukiwa tutafunga mwaka na pengine miradi haijakamilika, zile pesa bado huwa zinarudishwa. Sasa ukiona mradi wa 2021 mpaka sasa haujakamilika lazima ujiulize pesa zake zilienda wapi? kwa sababu lazima zilirudi na kama zilirudi, zilifanyiwa nini?

Bw. Spika, haya si majibu ya kwanza kuwa hayaridhishi ndani ya hii Bunge kutoka kwa ndugu zetu kule *Executive*. Nafikiri tumekuwa hapa tukipiga kelele; hakuna jibu limetoka kutoka ule upande wa serikali ambalo limeridhisha mwenye kuuliza ama hili Bunge. Hii inamaanisha nini Bw. Spika? Pengine utuelekeze ikiwa hatujaridhika na si mara ya kwanza hata yale maswala ambayo yameulizwa huko nyuma, watu bado hawajaridhika na yanaachiliwa. Je, kuna njia gani nyengine ya kuhakikisha kuwa wameleta majibu ambayo hayaridhishi? Tunaweza kuchukua hatua gani ndio tuhakikishe wanaleta majibu ambayo tumeridhika? Ikiwa umeuliza swala halafu tegemeo lako ni kuwa upate jibu ambalo pia wewe wananchi wako ambao wamekuleta hapa utawapatia hilo jibu.

Hivi sasa, kwa mfano mheshimiwa Koki unaenda kujibu nini au kuambia watu wako nini kulingana na hili jibu la Waziri? Kwa hivyo, Bw. Spika, tunahitaji mwelekeo kujua ikiwa jibu limeletwa na haliridhishi tunachukua hatua gani nyengine ili watu wawe watapata majibu ya kuridhisha na sio kuturidhisha sisi kama Bunge lakini kuhakikisha kwamba miradi inatekelezwa. Wewe ni jirani yangu na kwako tayari kuna shida kama hizi mimi naziona. Kwa hivyo, hata wewe, Bw. Spika, haya maswala yanakuhusu sana na kila mtu.

Hata mimi ukisema sina Wadi lakini nimeletwa na chama na kuna watu nawawakilisha na watu wako ndani ya hii Kaunti ya Kilifi. Nikisimama hapa nazungumzia kwa wale watu wote ambao tunawakilisha sio Wadi moja. Imefikia mahali kwa sababu tunataka kushika mwaka wa tatu na kama kila siku tutakuwa tunapewa majibu ambayo hayaridhishi na bado tutakuwa tunauliza maswali inavunja moyo sana hata inafikia wakati unaona hata haina haja pia ya kuuliza. Lazima tutafute mbinu, Bw. Spika, na asante kwa kunipa fursa hii.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Mariam, nilikuwa nataka nikukumbushe ndiposa nikasema *Statement* ya mheshimiwa Koki sio ya Wadi ya Mariakani peke yake lakini ni ya kaunti nzima ya Kilifi. Kwa hivyo, nataka nikupongeze kwa kutoa mwito kwamba tushikane ili kwamba tatizo kama hili liwe litarekebishwa katika Wadi nyengine pia. Asante. Mheshimiwa Hinzano ni wakati wako.

**Hon. Hinzano:** Asante sana, mheshimiwa Spika. Kabla sijaendelea ni kwamba ufahamu jambo moja ukiwa katika hicho kiti ni kwamba hauoni kwa hivyo kile kitu ninachokuomba ni kutupatia nafasi ili tuweze kuongee yale mambo ambayo yametuleta na kuweza kuyachagia ili wananchi waweze kutufahamu vyema na kuchangia.

Nikirudi katika majibu haya yaliyoletwa katika Bunge hili, haya majibu hayaridhishi. Mimi naona yanalingana na vile tunajibeba katika Bunge hili. Wameshatusoma kwamba wanaweza wakatumbea vile wanataka kwa sababu sisi wenyewe tukiwa waheshimiwa hatujibebi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*



kama ambaye tuko na mamlaka juu yao ndiposa wanajibu vile wanavyotaka wenyewe. Hakuna majibu yaliyofika hapa na mheshimiwa akasema ninaridhika na yanakuja kila wakati.

Nataka niwapatie mfano rahisi sana. Hii Kamati inayoongozwa na mheshimiwa Zia, walipoenda kuandika hiyo Ripoti yao na ikiwa pengine walikuwa na wasi wasi wanaweza wakakaa vizuri, wakaibadilisha ndio wailete hapa; ni aibu kubwa mtu analeta Ripoti hapa yeye mwenyewe alafu aitoroke anashindwa kusimama nayo. Sasa, unatarajia jamii ya Kilifi ikuchukulie vipi ikiwa wewe mwenyewe inaonyesha ya kwamba hujifahamu? Ikiwa utaleta Ripoti uwe wa kwanza kuiweka katika Bunge hili kwa mjadala halafu wewe mwenyewe uitoroke hutaki iendelee unabebaje hili Bunge? Mimi ...

*(The Deputy Speaker stood in his place)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Hinzano, naomba ukae chini. *When the Speaker is on his feet, you are supposed to sit down.* Kitu ambacho kiko, mheshimiwa Hinzano, tulikuwa tunatarajia utoe maoni yako kuhusiana na majibu yaliyotoka...naomba ukae chini sijakupa ruhusa...

*(Hon. Hinzano took his seat)*

...na kusimama kuacha ku *attack* mheshimiwa wa Kamati ambayo haihusiki na hili jambo sio sawa. Kwa hivyo, unajua na hata mheshimiwa Zia aliposimama akasema wazi kwamba saa hii anaendelea vizuri. Wakati huo ujue ya kwamba kama mheshimiwa Zia hayuko, sisi sote tunajukumu moja la kubeba msalaba kama kuna Hoja imeletwa ni jukumu la waheshimiwa wote na Bunge hili kulibeba sio jukumu la mtu binafsi. Asante.

**Hon. Hinzano:** Nachangia kwa Mada tena nachangia kwa mpangilio ambao utatufanya sisi tuende mbele. Mheshimiwa Spika, mimi nimemtaja mheshimiwa Zia kwa sababu yeye ndio Mwenyekiti wa hiyo Kamati. Yeye ndio anaongoza hiyo Kamati na wale aliowapata kuleta huu Mswaada bila shaka walishauriana na Mwenyekiti. Kwa hivyo, sijaambia mheshimiwa Zia kwa sababu najua alikuwa ni mgonjwa.

Ukiangalia kwa makini...

*(Hon. Zia stood on a Point of Order)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Zia, nakupatia nafasi. Kaa chini mheshimiwa Hinzano.

**Hon. Zia:** Asante sana, mheshimiwa Spika. Nakosa kuelewa vile majadiliano yanaendelea kwa sababu nafikiri mada ambayo iko mbele yetu ni kuhusiana na swala ambalo aliuliza mheshimiwa wa Mariakani. Leo hii hapa inajadiliwa Ripoti ambayo tayari ishahitwa na wakati ya Kamati ya Ugatuzi. Wakati huo hiyo Ripoti ikiletwa hapa, mimi nilikuwa niko hospitali ikiwa nina ugua. Nataka kuweka wazi kwa sababu wananchi wa Adu wananiangalia wakijua kwamba vile inasemekana ni kwamba nilikimbia hiyo Ripoti mimi mwenyewe na akaongezea kusema inatuonyesha nini? Sasa ni kama mimi sijielewi na nataka niweke wazi ili wananchi wa Kilifi na wakaazi...

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Zia, naomba ukae.

**Hon. Zia:** No! Haiwezekani, lazima nijitete. Nilikuwa mgonjwa...

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Zia, kaa chini na ukiendelea kuongea tutachukua hatua.

**Hon. Zia:** Tumesikia lakini inaudhi.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Zia, Order! Nimekupa heshima na nilikuwa nimekutetea vya kutosha. Ukifanya hivyo tena hatutakuwa na huruma na wewe tena.

**Hon. Zia:** Nisamehe. Asante, lakini asirudie.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa aliyekuwa katika Sakafu aendeleo.

**Hon. Hinzano:** Asante sana, nimepata ufahamu kuwa kumbe kusoma sio kuelimika. Mheshimiwa, majibu ambayo yako juu ya swali la mheshimiwa Koki yanaudhi sana. Elimu ndio msingi wa jamii yetu, hiyo basi kuna mahali tunaanzia ambayo ni hizi shule za chekechea (ECDE). Kama Waziri atatoa majibu kama haya ni wazi kwamba tunaanza kupotea kama Kaunti.

Mimi niko katika Kamati ya Elimu na haya mambo tuliyazungumza kwa kina sana; juu ya hii miradi ambayo imekwama. *Chief officer* na Waziri wakatuhakikishia kwamba kila kitu kitakuwa sawa. Sasa hivi majibu ni haya ambayo hayaridhishi Bunge hili. Kama wanaona hawawezi kujibu basi wanyamaze kuliko kujibu tu. Lazima tuwe na msimamo na mwelekeo ili wafahamu kuwa tuko na mamlaka tuliyokabidhiwa na wananchi.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Mheshimiwa Hinzano, nataka ujue kwamba wewe una mamlaka na ni jukumu lako kuhakikisha kwamba hili jibu ambalo limeletwa katika Bunge hili ni la hakika.

**Hon. Juma:** Asante, Bw. Spika, kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika mjadala ambao oko mbele yetu. Kwa niaba ya watu wa Mnarani naomba niseme hivi, nakubaliana na Mheshimiwa Martha Koki kutoka Wadi ya Mariakani. Mambo yanayozungumzwa ni ukweli na pia nakubaliana na mheshimiwa wa Kakuyuni. Jambo la kunishangaza ni kwamba jambo moja linachukua miaka na ni jambo linajirudia; kisu cha kukata huyu mnyama tuko nacho sisi.

Kwa mfano kule kwangu kuna Takaungu ECDE; ilikamilika bado milango na madirisha. Cha kusikitisha zaidi, meza, viti na vifaa vingine ambavyo wanafunzi wangetumia vimewekwa mahali chini ya miti na kukinyesha inaharibu *furniture* hizo. Hizo *furniture* zingine tulipata kwa wafadhili; sasa kuna hatari kubwa kwamba tunaweza kuchukua muda kitambo tujengewe madarasa zile *furniture* zitakuwa zimekwisha oza na maji.

Nataka kuwapa changamoto waheshimiwa. Nina uhakika kila mmoja wetu yuko na asilimia 75 ya kujua ni mbinu gani ambazo tunaweza kuzifanya ili mambo haya yakatatamika. Tukifika hapa Bungeni hakuna yule ametoka kwa chama fulani au mrengo fulani ili mambo haya tuyaweke sawa. Kuna wakati mwingine unaona kama ambaye sisi wajumbe ambao tuko hapa ni kama wengine wanalenga wengine na kuwatilia maneno wengine. Nina uhakika kama tutajiweka vizuri kulingana na sheria tuangalie mbinu tofauti tofauti ili kumaliza jambo hili. Nawasisitiza wajumbe wenzangu; tunaweza kuongea hadi kukacha, tusiongee kufurahisha watu labda nani ananiona ama nimewatetea wakaniona halafu tukitoka hapo tunawacha. Hiyo haitasaidia na hata kama hatutaongea kama sheria ziko tufwate.

Kila mtu akae kwa Kamati yake na tufwate sheria na nawahakikishia tukienda hivyo sisi wenyewe tutakuwa mahali salama pia watu wetu watasaidiaka.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Wacha nimkaribishe mheshimiwa Munyoki atoe maoni yake na pia atufungie kwa upande wa maoni.

**Hon. Munyoki:** Asante sana, Bw. Spika. Nataka kumuunga mkono mjumbe wangu mheshimiwa Koki. Mimi ni mkaazi wa Mariakani. Mengi yameongewa lakini nitakubaliana na

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mheshimiwa Juma chengo; kwamba sisi kama wajumbe tuko na suluhu. Nikinukuu maneno ya mheshimiwa Hinzano, anasema yeye anakaa katika Kamati hiyo ya Elimu, wakikaa kama Kamati na kujadiliana kuhusu miradi hii yote ambayo imekwama kwa nini basi sisi kama Bunge tusiamue kumuita huyu Waziri aje hapa atueleze kinagaubaga ana mipangilio gani ama kama amelemewa pia aje hapa mbele ya Bunge atueleze pia. Tujue mipangilio yake ni ipi; maanake sasa tunazunguka na hatuna muelekeo na tutaongea mpaka kila mara inakuja miradi ile ile tukiongea. Tumuite hapa kwa Bunge aje hapa atupe majibu mwafaka. Je, ana mipangilio na mikakati ipi kusuluhisha hii shida? Hayo machache, mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa wakati huu.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Asanteni, waheshimiwa, kwa changizo zenu kuhusiana na huu majadala wa wakati huu. Jibu hili tunalirudisha kwa Kamati ya Elimu mlikalie vizuri mlijadili na mhakikishe kwamba tunapata jibu mwafaka kwa kilio ambacho kimetoka katika Sakafu ya hili Bunge. Asanteni. Twende kwa jibu la swali la pili.

#### STATUS OF ZIANI ECDE PROJECT

**Hon. Rashid:** Asante, mheshimiwa Spika. I am reading a Response. The second Response; Response to County Assembly Statement on Ziani ECDE (Early Childhood Development and Education) in Chasimba Ward. Kisimani Mkwajuni and Mwakuwawa ECDE project.

The letter: this letter is in reference to your communication dated 15<sup>th</sup> October 2024, reference number CAK/Department of Education/3/Vol.2/78 on the above subject matter. The Division of Education wishes to respond as follows: -

Number one; Ziani ECDE in Chasimba Ward. The above-mentioned project was an Executive project initiated in the financial year 2023/2024, awarded to a contractor for a contract sum of Kshs5,451,756.40. The project was handed over for commencement on 5<sup>th</sup> April 2024 but the contractor failed to begin the construction work. As a result, the Department initiated a termination process, and the contract was officially terminated on 19<sup>th</sup> September 2024. Copies attached.

The project does not have an allocation in the approved budget for FY 2024/2025. Funds will be allocated in the first supplementary budget FY 2024/2025 after which the project will be returned to another contractor for its completion. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Thank you, hon. Rashid Odhiambo, for the Response. Now, we give an opportunity to hon. Mbura to react to the Response. Place your request, please.

**Hon. Mbura:** Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Kwanza, nataka niseme *Statement* yangu na ya Mheshimiwa Koki ina tofauti ya uchache kidogo lakini ni kama ziko sawa. Yake yeye zilianza lakini zikakwama, yangu mimi mwanakandarasi alipewa kazi lakini hakuanza na si ya Chasimba pekee ni nyingi lakini niliona bora mimi niulize kwa niaba ya wote. Jambo linalonishangaza ni kwamba *projects* zile ambazo zimesimama ni nyingi sana na hizi ambazo pia hazijaanza pia ni nyingi.

Sijui kuna hakika gani kwamba *supplementary* ijayo huyu bwana ataweka hizi pesa, kwa sababu zile ambazo zaendelea hazina pesa, hizi ambazo hazikuanza kabisa anasema ndio atazirudisha kwa bajeti ili ziweze kutekelezwa. Sitaki niende mbali sana lakini kwa sababu ya *Statement* yangu na swali nililouliza ndani ya *Statement* naona kwamba hatua mwafaka wamefuata na wakafika mwisho wa kunieleza ni hatua gani watafanya mimi sitaki niwe mwingi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sana wa maneno. Nasema kwamba swali nililouliza katika *Statement* walilijibu na taratibu walizofanya, kwa hivyo naridhika kwa hilo jibu. Asanteni.

### ADJOURNMENT

**The Deputy Speaker** (Hon. Kombo): Waheshimiwa, nafikiri tumemaliza biashara ya leo asubuhi na tunatamatisha kipindi hiki na tutakutana tena hapo mchana saa nane na nusu kwa kipindi cha mchana. Asanteni.

The House rose at 10:38 a.m.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*